**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA**

S.L.P. 90397,
Simu Nambari: 0652409165
Nukushi:(022) 2170963
Barua Pepe:
rbckinondoni@pccb.go.tz
Wavuti:www.pccb.go.tz

**KINONDONI, MEI 2022**

## MANISPAA KINONDONI YALALAMIKIWA KWA KUCHELEWESHA KUKAMILISHA ZOEZI LA URASIMISHAJI NA KUTOA HATI MILIKI.

**Ndugu wana habari;**

Ni wakati wetu mwingine tena, ambapo Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa –TAKUKURU Mkoa wa Kinondoni, tunatoa taarifa kwa umma kuhusu utendaji kazi wetu kwa kipindi cha miezi mitatu kupitia kwenu, kama ulivyo utaratibu wetu wa kawaida. Mnakaribishwa sana katika mkutano huu kwa ajili ya kufanya kazi hii muhimu sana kwetu na kwa wananchi wote kwa ujumla.

Katika kipindi cha kuanzia Januari hadi Machi 2022, TAKUKURU Mkoa wa Kinondoni imeendelea na majukumu yake ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa kulingana na Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Namba 11 ya Mwaka 2007 na imefanikiwa kutekeleza mpango kazi wake katika Idara zote ambazo ni Uchunguzi, Uzuiaji Rushwa na Elimu kwa Umma.

**Ndugu Wanahabari,**

**Uchunguzi:**

Katika kipindi hicho, TAKUKURU Mkoa wa Kinondoni imepokea jumla ya taarifa **mia sitini na moja (161).** Kati ya taarifa hizo, taarifa zinazohusiana na vitendo vya Rushwa zilikuwa **Themanini na moja (81)** na zisizohusu masuala ya Rushwa ni **Themanini** (**80**).

Katika taarifa hizo **81** zilizohusu rushwa**,** tumefungua majalada ya uchunguzi ambapo majalada yaliyofunguliwa na kufikia hatua ya uchunguzi wa kina ni **Kumi na moja** (**11**) na jalada moja (**1**) limekamilika na kwenda Ofisi ya Taifa ya Mashtaka. Majalada **69** yaliyobaki, uchunguzi wake bado unaendelea. Malalamiko 80 ambayo hayakuhusu rushwa, watoa taarifa walielimishwa na kushauriwa namna bora ya kushughulikia malalamiko yao.

Mchanganuo wa kisekta wa malalamiko **161** yaliyopokelewa ni kama ifuatavyo: Asasi Binafsi taarifa **68**, TAMISEMI taarifa **24,** Ardhi **15,** Polisi **14,** Mahakama **13**, TBS **11** na malalamiko **16** yalihusu mtu mmoja mmoja.

Katika kipindi husika, **kesi mpya moja (1)** imefunguliwa katika Mahakama ya Wilaya Kinondoni na kufanya jumla ya kesi zinazoendelea mahakamani kuwa kesi **Kumi na mbili** (**12)**. Kesi moja (**1**) imetolewa hukumu na Jamhuri imeshinda.

**Ndugu wanahabari**;

**Uelimishaji Umma:**

TAKUKURU Mkoa wa Kinondoni iliendelea na jukumu la kuelimisha umma kupitia njia mbalimbali, lengo likiwa ni kuwahamasisha wananchi kushiriki kwa vitendo katika mapambano dhidi ya rushwa.

Uelimishaji ulifanyika kwa kuendesha semina kumi na moja (**11**) kwa makundi mbalimbali na mikutano ya hadhara minne (**4**).

Pia tumeshiriki katika maonesho Manne (**4**) tumeimarisha klabu za wapinga rushwa kumi na saba (**17**) na kufanya kipindi cha TV kimoja (**1**).

Vilevile TAKUKURU Wilaya ya Ubungo kwa kushirikiana na Kamanda wa Skauti Wilaya ya Ubungo walitambulisha mwongozo wa mafunzo kwa wawezeshaji kufundisha vijana wa Skauti kuhusu kuzuia na kupambana na Rushwa na walitoa elimu kwa vijana wa skauti pamoja na walimu walezi wa klabu za wapinga Rushwa katika shule ya Sekondari Mabibo, Shule ya Sekondari King'ong'o, shule ya Msingi Mburahati,Shule ya Sekondari Babro, Shule ya Msingi Mugabe, Shule ya Msingi Mabibo, shule ya Msingi Milenia ya tatu, shule ya sekondari Kiluvya na Shule ya msingi Msewe kwenye ukumbi wa TGNP Mabibo tarehe 19/03/2022 ikiwa ni muendelezo wa ushirikiano wa mafunzo kati ya Takukuru na Skauti.

Mwongozo huo wa mafunzo unatokana na mkakati uliopo kati ya TAKUKURU na Chama cha Skauti Tanzania ambao ulizinduliwa rasmi Machi, 2020. Mkakati huu wa TAKUKURU na Skauti (TAKUSKA), ni sehemu ya utekelezaji wa Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa na Mpango wa Utekelezaji Awamu ya Tatu ambao lengo lake ni kuwaongoza wawezeshaji ili wawafundishe vijana wa Skauti kuwa waadilifu, wawajibikaji na wazalendo kuanzia ngazi yake binafsi, katika familia, shuleni, jamii na Taifa.

**Ndugu Wanahabari,**

Katika kufanikisha mpango wa TAKUKURU INAYOTEMBEA, kipindi hiki tulishirikiana na ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Dar es salaam na Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Kinondoni, kuelimisha wananchi katika Kata ya Mabwepande Mtaa wa Nyakasangwe waliokuwa na mgogoro wa ardhi katika eneo lenye hekta 1,199 kati ya wavamizi na wananchi wamiliki wa maeneo hayo. Baada ya kukaa pamoja na kujadili, tulifikia maamuzi ya kuwa kwa wavamizi ambao wameendeleza maeneo ambayo wamevamiwa, wayanunue maeneo hayo kwa bei ya sh. 8,500/= kwa square meter moja na fedha hizo zitalipwa kwa wamiliki wa awali wa maeneo hayo yaliyovamiwa.

TAKUKURU mkoa wa Kinondoni pia ilielimisha Watumishi wa Idara ya Biashara, Utawala na Kitengo cha Manunuzi Manispaa ya Kinondoni,

kuhusu Maadili na Makosa ya Rushwa mahali pa Kazi. Uelimishaji huo ulifanyika tarehe 19 Februari 2022 kwa lengo la kuwapa elimu ya mapambano dhidi ya Rushwa watumishi wa Manispaa na kuwakumbusha kufuata maadili ya kazi na kuzuia Rushwa katika kufanya kazi zao za kila siku.

**Ndugu wanahabari**;

**Uzuiaji Rushwa:**

Katika kipindi cha mwezi Januari hadi Machi 2022, ofisi ya TAKUKURU Mkoa wa Kinondoni ilifanya ufuatiliaji wa miradi wenye thamani ya sh **11,229,118,775.25.** Miradi huu ni mradi wa ujenzi wa Barabara ya Mkwajuni hadi Mbweni. Lengo la ufuatiliaji wa miradi hii ni kuhakikisha kuwa fedha zinatumika kwa usahihi kama ilivyoelekezwa kwa kuzingatia ubora, thamani ya fedha na muda husika.

Pia TAKUKURU Mkoa wa Kinondoni ilifanya ufuatiliaji wa utekelezaji wa maazimio ya kikao cha uchambuzi wa mfumo wa mianya ya rushwa katika usimamizi wa mitihani katika vyuo vya kati na ufuatiliaji wa utekelezaji wa maazimio ya kikao cha uchambuzi wa mfumo wa mianya ya rushwa katika utoaji wa vibali vya ujenzi katika Manispaa ya Kinondoni. Lengo la kufanya ufuatiliaji huo ni ili kujua kama yale yaliyoazimiwa kwenye kikao hicho yamefanyiwa kazi na mianya ya Rushwa iliyokuwa imebainika imezibwa kwa kufanya marekebisho kwenye mifumo yao.

Aidha, TAKUKURU Mkoa wa Kinondoni ilifanya **warsha (2)** ambazo hufanyika baada ya Uchambuzi wa Mfumo. Warsha hizo ni Warsha na wadau wa urasimishaji wa makazi iliyofanyika katika ukumbi wa mkutano wa TAKUKURU Mkoa wa Kinondoni na katika warsha hiyo ilijadiliwa tatizo la Uchelewaji wa kupata HATI MILIKI kutoka Manispaa kwa wananchi ambao wamekwisha kamilisha taratibu zote na malipo ya hati miliki na pia ilijadiliwa tatizo la idadi ya wananchi waliofanyiwa urasimishaji kuwa ni kubwa kuliko hati miliki zinazotolewa.

Baada ya kufanyika majadiliano hayo, tuliwekeana maazimio ya namna ya kutatua matatizo hayo yaliyobainika na kupatiwa muda wa kufanya marekebisho ili matatizo hayo yasijirudie.

Pia ilifanyika warsha ya usimamizi wa mitihani katika Chuo cha Kilimanjaro (KITM) baada ya kuchambua mfumo huo, ilibainika kuwa kuna mianya ya rushwa katika utunzaji wa mitihani kwa Examination Officer kwa muda mrefu na hivyo kupelekea kuwa na vishawishi vya kutaka kuuza mitihani hiyo kwa watahiniwa. Pia ilibainika kuwa tatizo lingine ni kabati la kutunza mitihani hiyo siyo imara sana na hivyo kupendekeza muda wa mitihani kutunzwa kwa Examination Officer upunguzwe na kabati imara la chuma la kutunzia mitihani hiyo linunuliwe na kuwe na kufuli na funguo ambazo zitatunzwa na uongozi.

**Ndugu wanahabari,**

## MIKAKATI KWA KIPINDI CHA APRILI – JUNI 2022

Katika kuhakikisha kuwa TAKUKURU Mkoa wa Kinondoni inatoa huduma inayowafikia wananchi wote, tutaendelea na utaratibu wa kutenga siku maalumu ya kusikiliza malalamiko na kero za wananchi kwa kuwafuata maeneo mbalimbali chini ya mpango wa TAKUKURU INAYOTEMBEA.

Hatahivyo tunapenda kuwajulisha wananchi kwamba ofisi zetu hapa Mkoani na Wilaya ya Ubungo kila siku ya Alhamisi ya mwisho wa mwezi tunasikiliza kero za wananchi.

Vilevile, tutaendelea kushirikiana na Chama cha Skauti chini ya mpango wa TAKUSKA, katika mapambano dhidi ya rushwa. Katika kutekeleza mkakati tuliojiwekea, tunatarajia katika kipindi cha Aprili hadi Juni 2022, tutatoa elimu ya mapambano dhidi ya rushwa ikiwemo umuhimu wa ufuatiliaji wa miradi ya maendeleo kwa vijana wa Skauti na Klabu za wapinga rushwa.

## HITIMISHO

TAKUKURU Mkoa wa Kinondoni tunaendelea kutoa wito kwa wananchi wote katika mkoa wetu kuendelea kutoa ushirikiano kwa TAKUKURU na pia kuepuka matapeli wanaoibuka na kuwapigia simu wananchi kwa kujifanya wao ni maafisa wa TAKUKURU, huku wakiwatapeli kwa kuwatisha kuwa wana tuhuma zao - hivyo kuwadai pesa ili wawasaidie kuzifuta tuhuma hizo.

Tunawasihi wananchi wote kuwa mpatapo taarifa zozote za rushwa na matapeli kama hao kutoa taarifa kupitia mitandao yote ya simu kwa kupiga au kutuma ujumbe mfupi kwa namba ya dharura **113 –** BURE, na kufuata maelekezo au kufika katika ofisi yoyote ya TAKUKURU iliyopo karibu nawe.

**"KUPAMBANA NA RUSHWA NI JUKUMU LANGU"**

Imetolewa na:

**Donassian N. Kessy**
**Mkuu wa TAKUKURU (M)**
**Kinondoni**
**0738150236**